

Sera ya Kuazima Vitu
Mfumo wa Maktaba wa Kaunti ya Lancaster

Ustahiki wa Kadi ya Maktaba

Kadi ya muazimaji binafsi

Kadi ya maktaba ya Mfumo wa Maktaba wa Kaunti ya Lancaster itatolewa bure kwa mkazi yeyote wa Kaunti ya Lancaster mwenye miaka mitano au zaidi.

Mtoto aliye chini ya miaka 14 lazima fomu yake ya maombi ya kadi ya maktaba isainiwe na mzazi au mlezi halali atakayewajibika kwa kufuatilia nyenzo zilizoazimwa na mtoto, pamoja na faini za mtoto na gharama ya nyenzo zozote zitakazopotea au kuharibiwa. (*Angalia Sera ya Usiri hapo chini*)

Waombaji wote watapaswa kutoa uthibitisho wa ukazi kupitia moja ya vyanzo vifuatavyo:

- Leseni halali ya udereva au Kitambulisho chenye Picha cha Jimbo
- Kitambulisho cha hivi sasa
- Bili ya kampuni inayotoa huduma muhimu au duka inayomtambulisha mhusika ya miezi mitatu iliyopita
- Bili ya kodi ya majengo
- Hati za kufanya kazi zilizotolewa kwa kijana
- Nakala ya pango au hati ya hivi sasa
- Hundi zenye anwani iliyochapishwa awali
- Kitambulisho halali cha chuo / chuo kikuu cha Kaunti ya Lancaster

Ada ya mwaka ya \$25.00 itatozwa kwa watu wasio wakazi wa Kaunti ya Lancaster. Hata hivyo, watu wenye kadi ya sasa ya maktaba yenye stika ya "Access Pennsylvania" ya maktaba yao ya nyumbani hawatatozwa ada. Watu wasio wakazi ambao hawan kadi ya sasa ya maktaba yenye stika ya "Access PA", lazima walipe ada ya mwaka.

Baadhi ya maktaba zinatoa vibali vya wageni kwa wasafiri na watu wasio wakazi ili kutumia rasilimali hapo hapo maktaba. Uliza mapokezi ya maktaba wanachama kuhusu kanuni zao za ndani.

Kujiandikisha Mwenyewe Mtandaoni (OSR)

Huduma ya OSR inapatikana kwa:

- Wakazi wa Kaunti ya Lancaster, Pennsylvania.
- Watumiaji wenye miaka 14 na zaidi

Nambari ya OSR ni halali kwa miezi 3 na haiwezi kutolewa upya na haiwezi kurejeshwa. Watumiaji lazima wafike au wawasiliane na maktaba mahalia ili kupandisha daraja la kadi ya maktaba kuwa yenye ufikio kamili. Watumiaji lazima wajaze makaratasi yote ya maombi katika maktaba na kutoa uthibitisho wa ukazi ili kupandisha daraja.

Nambari yako ya OSR **inaweza** kutumika:

- Kuazima [eBooks na eAudiobooks](#)
- Kuweka zuio la vitu halisi vya maktaba
 - Ili kuchukua vitu vyako vilivyozuiwa, lazima ufike au uwasiliane na maktaba yako mahalia ili kupandisha daraja kadi yako ya muda kuwa kadi yenye ufikio kamili.
- Kutumia [Rasilimali za Mtandaoni](#)
- Nambari yako ya OSR **haiwezi** kutumika:
 - Kuazima vitu halisi vya maktaba
 - Kutumia kompyuta za umma kwenye maktaba

Kadi ya Taasisi

Kadi ya taasisi ya maktaba inatolewa kwa shirika lililopo Kaunti ya Lancaster ambalo litawajibika kwa nyenzo zote zilizoazimwa. Maombi lazima yaambatane na barua yenye anwani ya shirika linaloomba kadi ya maktaba, na kukubali kuwajibika kwa nyenzo zote zitakazoazimwa na maombi hayo yatasainiwa na mkurugenzi wa shirika hilo. Faini za uchelewaji zitatozwa kwa nyenzo zozote ambazo hazitarejeshwa kufikia tarehe husika. Vipindi maalum vya uazimaji vinaweza kupangwa kwa ombi.

Matumizi ya Kadi ya Maktaba

Kadi ya maktaba ya Mfumo wa Maktaba wa Kaunti ya Lancaster inaweza kutumika katika maktaba yoyote ya umma ambayo ni mwanachama wa Mfumo wa Maktaba wa Kaunti ya Lancaster.

Haki ya uazimaji inaweza kuondolewa kwa sababu kadhaa, ikiwemo, lakini haikomei kwa, kushindwa kurejesha vitabu vilivyocheleweshwa, kushindwa kulipa faini za uchelewaji, na kushindwa kulipia nyenzo zitakazopotea au kuharibiwa.

Watumiaji wa maktaba wana wajibu wa kutaarifu maktaba yoyote mwanachama kuhusu badiliko la anwani ndani ya siku 30.

Kadi za maktaba zilizopotea au zilizoibiwa lazima ziripotiwe katika maktaba yoyote baada tu ya kujua. Kadi zitarudishwa kwa \$1.00.

Usajili wa Watumiaji

Taarifa zifuatazo zitahifadhiwa kwa usalama kama sehemu ya usajili wa watumiaji:

- Jina, Anwani, Nambari ya Simu
- Manispaa ya makazi
- Wilaya ya Shule

Taarifa zifuatazo zitaombwa wakati wa usajili, lakini zitakuwa za **hiari** kwa upande wa mtumiaji:

- Tarehe ya kuzaliwa (inahitajika kwa watoto)
- Anwani ya Barua pepe
- Kitambulisho chenye picha cha kielektroniki kwa ajili ya rekodi ya mtumiaji

Vipindi vya Kuazima Vitu

- Vipindi vya uazimaji vinatofautiana kulingana na makusanyo, eneo na muundo.
- Kwa kawaida, Video, DVD, Vinavyohitajiwa Sana / Vilivyouzika Sana huazimwa kwa wiki 1
- Nyenzo nyingine zote huazimwa kwa wiki 2

Kuazima Tena Nyenzo za Maktaba

Kuazima tena kunaweza kufanywa mapokezi ya maktaba mwanachama, kwa simu au mtandaoni.

- Kuazima tena katika mapokezi ya maktaba mwanachama kunahitaji vitu au kadi ya maktaba iliyotumika kuazimia vitu hivyo. Kuazima tena kwa simu kunahitaji nambari ya kadi ya maktaba.
- Kuazima tena kwa njia ya Intaneti kunapatikana kwa kuingia Katalogi ya Mtandaoni ya Mfumo wa Maktaba wa Kaunti ya Lancaster. <https://search.lancasterlibraries.org/>
- Baadhi ya sababu za kutoazimwa tena kitu ni: muazimaji mwingine ameomba kitu hicho; nyenzo ya aina hiyo haistahiki kuazimwa tena; umefikia ukomo wa kuazima tena kitu hicho; au, kwa sababu ya faini za uchelewaji kwenye rekodi yako. Ikiwa huwezi kuazima tena vitu vyako, tafadhali piga simu maktaba yako mahalia.

Sera ya Kuazima Vitu
Mfumo wa Maktaba wa Kaunti ya Lancaster

- Kwa Uazimaji Tena wa ILL, angalia sera ya ILL

Zuio

Watumiaji wa maktaba wanaweza kuweka ombi ('zuio') la hadi vitu vitano vya maktaba za umma ndani ya Kaunti ya Lancaster. Zuio linaweza kuwekwa mtandaoni kwa kuingia katika:

<https://search.lancasterlibraries.org/> kwa simu, au kwa usaidizi wa mfanyakazi wa maktaba mapokezi.

Vitu vinapokuwa tayari kuchukuliwa, mtumiaji atataarifiwa kwa simu au kwa barua pepe.

Watumiaji wana siku saba za kuchukua vitu walivyoomba. Zuio ambalo halitachukuliwa ndani ya kipindi hicho litaondolewa.

Si vitu vyote vina ustahiki wa zuio. Hivi ni pamoja na, lakini havikomei kwa vitu vipya vinavyomilikiwa na maktaba

Kando ya maktaba ya nyumbani ya mtumiaji na vitu vilivyo katika makusanyo au miundo maalum.

Faini na Ada

Faini na ada zinaweza kulipwa katika maktaba yoyote ya Kaunti ya Lancaster au kwa kuingia:

<https://search.lancasterlibraries.org/> Faini zilizo chini ya \$3.00 hazina ustahiki wa malipo ya kadi.

- Senti 30 kwa siku kwa nyenzo za Watu Wazima na Vijana na faini isiyozidi \$5.10 kwa kila kitu.
- Senti 20 kwa siku kwa nyenzo za Watoto na faini isiyozidi \$3 kwa kila kitu
- \$1 kwa siku kwa Video na DVD zote na faini isiyozidi \$5 kwa kila kitu
- Kama ilivyoanishwa katika vitu vya miundo maalum.

Notisi za Uchelewaji

Ukumbushaji unaweza kutolewa kwa watumiaji walioweka barua pepe halali na waliokubali kupokea arifa za barua pepe.

Notisi ya Kwanza katika Wiki 2

Notisi ya kwanza ya uchelewaji itatumwa kwa anwani ya hivi karibuni zaidi au barua pepe halali iliyopo katika rekodi za maktaba ya akaunti ya mtumiaji ikiwa kitu kimechelewa kwa wiki 2. Notisi itajumuisha orodha ya nyenzo zilizochelewa.

Kushindwa kurejesha vitu husika vya notisi hii ndani ya siku kumi na nne (14) za kazi baada ya tarehe ya notisi hii itasababisha kuondolewa haki ya uazimaji ya mmiliki wa kadi katika kila maktaba ya Kaunti ya Lancaster hadi akaunti itakaposhughulikiwa.

Kushindwa kurejesha vitu hivi ndani ya wiki 4 baada ya tarehe halisi ya mwisho itasababisha akaunti ya mmiliki wa kadi kutozwa gharama ya ununuzi wa nyenzo husika.

Notisi ya Pili: Bili ya ununuzi baada ya wiki 4

Notisi ya pili inatumwa baada ya bidhaa kuchelewa kwa wiki 4. Hii ni bili ya ununuzi wa vitabu. Ikiwa vitu vilivyotozwa vitapatikana, utalipa tu faini ya uchelewaji.

Vitu Vilivyopotea na Kuharibiwa

Tozo ya vitu vilivyopotea ni sawa na bei ya kitu. Ni wajibu wa mtumiaji wa maktaba kuwasiliana na maktaba ili kuweka mipango ya malipo ya faini za uchelewaji. Maswali yoyote kuhusu ada za ununuzi wa vitu yanaweza kuelekezwa kwa maktaba inayodai.

Sera ya Kuazima Vitu
Mfumo wa Maktaba wa Kaunti ya Lancaster

Shurutisho la Faini za Uchelewaji

Watumiaji wa maktaba wanatarajiwa kurudisha nyenzo za maktaba mara moja na kulipa faini zozote za uchelewaji.

- Faini zaidi ya \$6.00 itasababisha kuondolewa haki ya uazimaji na ufikio wa rasilimali za mtandaoni.
- Kitu kikichelewa kwa zaidi ya siku 28, haki ya uazimaji inaondolewa hadi nyenzo zirejeshwe na faini ya uchelewaji kulipwa. Haki ya uazimaji na ufikio wa rasilimali za mtandaoni itarejeshwa baada ya jumla ya faini na ada kushuka chini ya \$6.00.
- Faini lazima zilipwe na nyenzo zilizochelewa zirudishwe kabla ya haki ya uzimaji kurejeshwa.

Usiri

Sheria ya Jimbo la Pennsylvania inasema:

Ibara ya 24 § 9375. Faragha ya rekodi za uazimaji.

Rekodi za taasisi zifuatazo zinazohusiana na uazimaji wa nyenzo za maktaba na zenye majina au taarifa nyingine binafsi za watumiaji wa nyenzo hizo zitakuwa siri na haziwezi kutolewa kwa mtu yeyote isipokuwa kwa amri ya mahakama katika kesi ya jinai:

Sera hii ya usiri inahusika kwa usawa kwa watu wazima na watoto. Mtu mzima anapoomba rekodi za mtoto, maktaba itajibu tu ikiwa mtoto huyo atakubali ombi hilo.

Imesasishwa: 08/2022